



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA



Kumb. Na.LD/MK/9398/21

15/4/2025

Mkurugenzi Mkuu
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)
S.L.P 6775,
Dar Es Salaam.

**YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA KERUI COMPANY LIMITED KUNUNUA
KIWANJA NA.98 KITALU 'H' KAZOLE, WILAYA YA MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu,

2. Ninachukua fursa hii kuijulisha Ofisi yako kwamba, kampuni tajwa hapo juu imenunua kiwanja tajwa na sasa wanatakiwa kusajiliwa na kupewa cheti cha usajili wa maradi na Ofisi yako.

3. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi **Na. 4 ya 1999, fungu la 19-20** sambamba na Sheria ya uwekezaji Tanzania **Na. 26 ya 1997**, kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), aidha kwa kuzingatia **fungu la 12 & 179 Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999** na Tangazo la Serikali **Na.72 la tarehe 4/5/2001**, Kanuni za Ardhi za 2001, **kanuni ya 9C (v)**, nawasilisha kwako fomu hii kwa hatua zaidi.

4. Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi kwako ili iweze kupatiwa Certificate of Incentive yenye kuonyesha namba ya kiwanja ili kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya kuandaa **Designation for Investment** (Land form Na. 1) ili kiwanja hiki kipelekwe katika kamati ya Ugawaji wa Ardhi Taifa kitangazwe kuwa cha uwekezaji

5. Naomba kuwasilisha kwa hatua zako muhimu

Riziki.M. Chagye
K.n.y: Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga.



Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga-----Kwa taarifa

✓ **Kerui Company Limited**
Dar es salaam--- kwa ufuatiliaji